Härnösands kommun

# Karibu kwenye shule ya msingi



**Je, ungependa kusikiliza?**
Hapa utapata broshua/kitabu nzima /kizima imegawanywa katika Sura au vipande. Sikiliza sehemu unayotaka.



## Shule ya msingi – ni nini?

Mwaka ambao mtoto wako anapotimiza miaka sita, anapaswa aanze darasa la shule ya awali/mapema. Baada ya darasa la shule ya awali, mtoto anaanza darasa la 1. Baada ya mwaka mmoja, anaendelea hadi darasa la 2 na kisha anaendelea hivyo hivyo mpaka darasa la 9.

Kwa watoto ambao hawawezi kuwa nyumbani wakiwa peke yao wakati ambapo wasaa wa shule umekwisha, lipo eneo la burudani kabla na baada ya masaa ya shule, au "fritids" kama vile linavyoitwa na watu wengi. Fritids hiyo ni kwa ajili ya watoto wenye umri kati ya miaka 6 mpaka 13, ambao wana wazazi wafanyao kazi au waendao masomoni.

Kwenye fritids, mtoto anapata kuwa pale zile siku ambazo hawako shuleni na wakati wa likizo. Mtoto hawezi kuwa katika fritids kwenye muda wa jioni, usiku, mwishoni mwa wiki au wakati wa wikendi. Isipokuwa, zipo zilizo maalum kwa watoto ambao wazazi wao wanafanya kazi nyakati za jioni, wikendi au usiku na hawana mtu mwingine wa kuwatunza. Kwa ajili yao inakuwepo hiyo maalum inayoitwa “nattis”. Soma zaidi kuhusu nattis kwenye tovuti la harnosand **harnosand.se/nattis.**

Haya yote, darasa la shule ya awali, darasa la 1-9 pamoja na fritids huitwa shule ya msingi.

Nchini Uswidi/Sweden haigharimu chochote kwenda shule. Endapo mtoto anahitaji kupata nafasi kwenye fritids, Manispaa/Kommun italipwa. Utapaswa kulipa kiasi gani itategemea kiwango cha mshahara unaopata.

Nyenzo au vifaa ambavyo watoto wanahitaji shuleni, kwa mfano vitabu, tableti za kusoma au kompyuta, wanaweza kuazima bila kugharimu chochote. Lakini ni muhimu kwamba watoto wanapaswa kuwa waangalifu na kila kitu wanachopata kuazima. Iwapo kwa mfano ile kompyuta ambayo mwanafunzi wa darasa la 7-9 anaruhusiwa kuazima, ikiharibika kwa kuvunjika au kupotezwa, wewe mzazi utalazimika kulipa.

## Wewe ni muhimu

Wewe kama mzazi, ni muhimu kwamba mtoto wako mambo yamuendee vizuri shuleni. Shule ingependa kuwa na mawasiliano na wewe pamoja na kuzungumza nawe kuhusu uwepo wa mtoto wako shule. Inafanyika hivyo ili kwamba ninyi kwa pamoja muweze kuufanya wakati wa shule uwe mzuri iwezekanavyo. Kwamba unajishughulisha na kushiriki katika kupokea taarifa kutoka shuleni, hakikisha kuwa mtoto wako amelala ipasavyo, amekula chakula cha asubuhi na kwamba amechukua vitu sahihi vinavyohitajika shuleni ni muhimu ili siku ya shule iwe nzuri.



## Elimu ya Lazima

Nchini Uswidi/Sweden, elimu ni ya lazima. Hii ina maana kwamba watoto inawapasa waende shule. Kama mzazi, unawajibika kwa mtoto wako kuja shuleni.

Endapo mtoto hafiki shuleni, lazima kuwe na sababu maalum, kwa mfano kwamba mtoto ni mgonjwa au kuwa amepewa muda wa mapumziko.

## Misimu ya mwaka wa masomo

Mwaka wa masomo daima unaanza baada ya majira ya joto/sommaren na unakuwa na muhula wa vuli/hösttermin pamoja na muhula wa masika/vårtermin. Muhula wa vuli unaanza mwezi wa agosti/mwezi wa 8 na unaisha mwezi wa desemba/ mwezi wa 12. Muhula wa masika unaanza mwezi wa januari/mwezi wa 1 na unaisha mwezi juni/mwezi wa 6. Tarehe kamili za kila mwaka wa masomo unazipata kwenye tovuti la harnosand chini ya kichupo watoto na elimu: **harnosand.se**



## Chagua shule

Kama mulezi na mzazi unaweza kupendekeza kuhusu shule gani ambayo ungependa mtoto wako asome. Unayo haki ya kupendekeza miongoni mwa shule zote zilizopo katika Manispaa nzima, lakini hakuna uhakika kwamba kuna nafasi kwenye shule uliyopendekeza. Hata hivyo, mtoto wako daima anayo haki ya kupata nafasi kwenye shule iliyopo eneo la karibu.

Je, ungependa shule tofauti ya manispaa kuliko ile iliyopo karibu na munapoishi? Basi lazima uwasilishe ombi la pendekezo lako moja kwa moja kwenye shule unayoipendekeza. Endapo mtoto wako ataanza darasa la shule ya awali, ombi la pendekezo la shule nyingine inapaswa liwasilishwe kabla ya tarehe 01 februari/ mwezi wa 2.

Katika manispaa ya Harnosand zipo shule za msingi za manispaa kumi na moja, moja ya kujitegemea pamoja na moja ya serikali kwa ajili ya viziwi na ulemavu wa kusikia.

## Jukwaa la kujifunza shuleni/Schoolity

Schoolity ni jukwaa la kujifunza lenye msingi wa tovuti ambalo wafanyakazi, wanafanuzi na walezi hutumia kuwasiliana wao kwa wao, kutazama mahudhurio na kutokuwepo pamoja na ratiba ya mwanafunzi. Jukwaa la kujifunza litarahisisha kazi ya kila siku ya wanafunzi na wafanyakazi shuleni. Inapaswa vilevile kufanya iwe rahisi kwako kufuatia shule ya mtoto wako. Inapatikana katika lugha ya kiswidi na kiingereza pamoja na kwamba unaweza kuchagua lugha mwenyewe.

Ili kuweza kutumia Schoolity unapaswa kuwa na maelezo ya namna ya kuingia kwenye hiyo tovuti. Soma zaidi kuhusu jinsi ambavyo utapata kwenye tovuti la **harnosand.se/schoolity**

Ikiwa unahitaji usaidizi kuhusu schoolity, unaweza kuwasiliana na kituo cha huduma cha manispaa ya Härnösand (Servicecenter).



## Kutokuwepo na ugonjwa

Kama mtoto wako hawezi kuja shuleni kwa sababu ya kwamba mtoto amekuwa mgonjwa, unapaswa kutoa taarifa hiyo shuleni. Unafanya hiyo ripoti kwa msaada wa Schoolity.

Lazima ufanye hiyo ripoti kwa kila siku ambayo mtoto hatokuwepo shuleni.

Ikiwa mtoto wako anahitajika kuondoka shuleni muda wowote wakati wa siku ya shule, kwa mfano kwenda kwa daktari au daktari wa meno, unapaswa kutoa taarifa hiyo kwa mwalimu wa darasa au mshauri/mentor.

## Pumziko

Kama mtoto wako anahitaji kupumzika kutoka shuleni, lazima uwasilishe ombi kwa wakati unaofaa. Hiyo unafanya kwa kutumia fomu inayopatikana kwenye tovuti la härnösand yaani harnosand.se. Mtoto wako hatopata pumziko ikiwa shule inaona kwamba muda wa kupumzika unaathiri kazi ya kitaaluma kwa njia hasi/mbaya.

Mwanafunzi hawezi kupewa mapumziko zaidi ya siku 10 katika mwaka wa masomo. Hii ina maana kwamba safari ndefu inapaswa zipangwe na kutekelezwa wakati wa likizo.

## Kutokuwepo batili

Shule inawajibika kufahamu mahali watoto wote wa shule waliko wakati wa saa za shule. Endapo mtoto wako hafiki na kwamba wewe haujatoa taarifa kwamba mtoto ni mgonjwa au haukuomba pumziko Iolote basi utapokea ujumbe ambao unaitwa kutokuwepo batili. Hii ina maana kuwa shule haina taarifa ya mtoto yaani hayupo shuleni muda huo.

Ni muhimu sana kwamba unakuwa makini katika kuarifu ikiwa mtoto wako ni mgonjwa au kwamba hatokuwepo shuleni kwa sababu nyingine yoyote. Kama

hakuna taarifa kutoka kwako inayohusu kwa nini mtoto wako hajaja shuleni, wafanyakazi watakutafuta hadi wamepata mawasiliano nawe. Kwanza kwa njia ya simu, barua-pepe/e-mail au ujumbe kwa simu/SMS pamoja na hatua nyingine itakayofuata ni kufika kukutembela nyumbani munapoishi. Ikiwa bado hawawezi kumpata mtoto au kufahamu kwa nini mtoto hayuko shuleni, hatimaye wanaweza kulazimika kuwasiliana na Polisi au ofisi ya huduma za Ustawi wa jamii.

Endapo mtoto hajakuwepo sana, shule itawasiliano nawe kwa ajili ya mazungumzo.

## Sheria ya shule na mtaala

Katika sheria ya shule kunaelezwa kuhusu haki na wajibu gani ambao watoto, wanafunzi na walezi wanayo. Kwenye sheria pia inaeleza ni masharti gani yanawekwa kwa mtu anayehusika na shule, mhusika mkuu wa shughuli nzima.. Kutokana na kuwa mtoto wako anasoma shule ya manispaa, manispaa ya Härnösand ndiyo mhusika mkuu.

Bodi ya elimu nchini ni mamlaka ya Serikali ambayo inaamua watoto watajifunza nini shuleni na watapata maarifa katika darasa gani. Walichoamua unaweza kusoma kwenye kitu kinachoitwa mtaala/Läroplanen.

Mtaala lazima ufuatwe na shule zote nchini Uswidi. Ni katika kutekeleza hili ambapo shule huweza kujenga na kuendeleza shughuli zao.

## Ukadiriaji/alama na tathmini

Katika darasa la 1-5, mwanafunzi anapata kinachojulikana kama tathmini katika kila somo kwenye muhula wa masika. Tathmini inayonyesha kama mwanafunzi amepita kiwango cha maarifa cha darasa husika.

Wanafunzi hupata alama zao za kwanza mwishoni kwenye muhula wa vuli katika darasa la

6. Kisha mwanafunzi hupata alama mpya kila muhula hadi majira ya masika katika darasa la 9 wakati alama za mwisho zinawekwa. Ni kwa kupitia hizo alama za mwisho ambazo zinamuwezesha mwanafunzi hatimaye kuomba kuendelea kwenye shule ya sekondari.

Kiwango cha uwekaji alama kinatoka kwenye A-F, ambapo A-ndiyo daraja la juu zaidi la ufaulu na F-daraja la chini maana yake ni kutofaulu.

## Afya ya mwanafunzi na usadiizi

Ikihusishwa na shule kuna kitu kinaitwa afya ya mwanafunzi. Inaweza kuhusisha tiba za dawa, kisaikolojia, kisaikolojia-jamii pamoja na juhudi za elimu maalum. Katika afya ya mwanafunzi wanafanyakazi Madakatari wa shule, Wauguzi/nesi wa shule, Wanasaikolojia na Washauri katika shule. Pia kuna Wafanyakazi wenye ujuzi maalum wa ufundishaji.

Wafanyakazi wa afya ya mwanafunzi uwepo wao unachangia kuwafanya wanafunzi kujisikia vizuri na kuwa na afya njema, kwa mfano kupitia mazungumzo ya afya na chanjo.

Kupitia afya ya wanafunzi, mtoto wako anapata, miongoni mwa mambo mengine, fursa ya kufanyiwa chanjo kwa mujibu wa mpango wa chanjo ya watoto nchini Uswidi. Ni chanjo ambazo zinakinga magonjwa kumi na moja: maambukizi ya rotavirus/tumbo la kuhara, donda koo, pepopunda/tetanasi, kifaduro, polio/kupooza, maambukizi yanayosababishwa na utando kooni aina b/haemophilus ambao ni ugonjwa hatari sana unaosababishwa na pneumococcus, surua, matubwitubwi, rubela pamoja na virusi vya papilloma ya binadamu (HPV).

## Masomo

Katika shule ya msinigi wanafunzi wanasoma masomo yafuatayo: kiswidi, kiswidi kama lugha ya pili, kiingereza, hisabati, picha/michoro, muziki, useremala, maarifa ya nyumbani, michezo na afya, maarifa ya kijamii, dini, historia, jiografia, elimu ya viumbe yaani biolojia, fizikia, kemia, ufundi, chaguo la mwanafunzi, lugha za kisasa ambapo mwanafunzi anachagua, kwa mfano kihispania, kijerumani au kiingereza pamoja na ufundishaji wa lugha-zazi katika zile-hali zenye utayari. Wanafunzi hawasomi masomo yote hayo kila siku, isipokuwa yanatofautiana kutoka muhula na mwaka.

## Kiswidi kama lugha ya pili (SVA)

Kiswidi kama lugha ya pili, SVA, ni somo tofauti, sawa na somo la kiswidi. Mwanafunzi mwenye lugha-zazi mbali ya lugha ya kiswidi wanaweza kuwa na haki ya kufundishwa katika SVA. Ufundishaji katika SVA unaweza ukahusisha mambo ambayo ni mahususi/ maalum katika kujifunza lugha ya pili, kwa mfano matamshi, mpangilio wa maneno na kulinganisha na lugha zote zingine za mwanafunzi. Ni shule inayoamua kama mwanafunzi ana haki na kwamba anahitaji kufundishwa katika SVA.



## Ufundishaji wa lugha-zazi na mwongozo wa kusoma katika lugha-zazi

Lugha-zazi ina umuhimu mkubwa katika maendeleo ya ukuaji wa mtoto katika lugha, mawazo, utambulisho na utu. Lugha-zazi iliyostawi vizuri inatoa hali nzuri ya kujifunza kiswidi, lugha zingine na masomo mengine.

Mtoto wako anaweza kupata mafundisho katika lugha-zazi yake. Ukitaka mtoto wako afundishwe lugha-zazi yake, unapaswa uwasilishe maombi kwenye sehemu husika. Unafanya hivyo kupitia huduma ya kielektroniki iliyoko kwenye tovuti ya manispaa ya Härnösand **harnosand.se/modersmalsundervisning**

## Michezo na kufundishwa kuogelea

Kuwa na mazoea ya kujichangamusha mwili katika muda wake huru kwa kutembea-tembea, ili kujenga afya ya mwili. Katika mitaala kuna somo la michezo na afya. Hali hii itampa mtoto wako mema ya uzoefu mzuri wa michezo, kujichangamusha mwili kwa kupenda kupata hewa safi katika mazingira ya nje. Katika mtaala vilevile imeandikwa kwamba mtoto wako anapaswa kujifunza kuogelea.

Watoto wote lazima washiriki katika masomo ya michezo na kuogelea. Wewe mzazi unao wajibu ulio muhimu inapohusu kuhakikisha kwamba mtoto wako anazo nguo za michezo, nguo za kuogelea na taulo katika zile siku ambazo mtoto anakuwa na somo la michezo shulen. Watoto wanapaswa kubadilisha nguo kabla ya somo la michezo na kisha kuoga baada ya kumaliza.

Ikiwa mtoto wako hawezi kushiriki katika michezo kwa sababu yoyote, lazima umjulishe Mwalimu.

# Mazungumzo kuhusu maendeleo ya mtoto na mikutano ya wazazi

Kila muhula shule inataka kukutana nawe mzazi. Mara moja katika muhula kuna mazungumzo ya maendeleo ya mwanafunzi. Basi hapo, wewe pamoja na mtoto wako munakutana na mwalimu au mshauri na munazungumza kuhusu namna maendeleo ya mtoto yalivyo shuleni.

Mara moja, katika mwaka wa masomo, mara nyingi mapema wakati wa majira ya vuli, kunakuwepo mkutano wa wazazi. Muda huo basi huwa shule inataka kukutana na wazazi wote darasani na kuwaeleza kuhusu shule na ule mwaka ujao wa masomo.

Endapo ungependa kuja na kutembelea shule, unakaribishwa kufanya hivyo. Lakini kabla ya kufanya namna hiyo, unapaswa kukubaliana na Mwalimu wa mtoto wako na utoe taarifa katika ofisi ya shule ya mapokezi pindi unapowasili pale.

# Chakula

Mtoto wako anapata chakula cha mchana shuleni. Chakula hicho cha mchana hakigharimu chochote. Katika shule nyingi, kuna aina mbalimbali za vyakula kadhaa vya kuchagua, pamoja na aina tofauti za mboga za majani. Watoto wanaohitaji lishe/chakula maalum kwa sababu za matibabu, kama vile mzio, wanaweza kupata ikiwa utawasilisha cheti cha daktari. Ikiwa mtoto ni vejiteriani, vegani au anahitaji chakula maalum kwa sababu za dini anayoabudu, unapaswa utoe taarifa shuleni, lakini hauhitaji kuwasilisha cheti, Angalia tovuti la Härnösand **harnosand.se/specialkost**

# Magari yanayowasafirisha watoto shuleni

Kama mtoto wako anaishi mbali na shule, endapo njia inayolekea shule ni ya hatari au ikiwa mtoto wako ana ulemavu, mtoto huyo anaweza kuwa na haki ya kusafirishwa na gari la shule.

Hii ina maana kwamba mtoto anaweza kupata usafiri kati ya nyumbani na shule bila gharama.

Magari yanayowasafirisha watoto shuleni, unaweza kuonekana tofauti. Yumkini mtoto wako anapata kadi ya Basi na kupanda Basi la kawaida, lakini pia inaweza kuwa Mabasi yaliyoagizwa maalum, Mabasi madogo au teksi. Taarifa zaidi zinapatikana katika tovuti la härnösand **harnosand.se/skolskjuts**

Kama umepata usafiri wa shule kwa mtoto wako na huduma haiwajibiki inavyotakiwa, unapaswa utume barua-pepe/ e-mail kwenda kwenye kitengo cha usafirishaji: **trafikenheten@harnosand.se**

## Simu tamba/simu za mkononi

Watoto kuanzia darasa la shule ya awali hadi darasa la 6 hatakiwi kutumia simu za mkononi wakati wanapokuwa shuleni. Kwa maana hiyo, shule wanataka kwamba

watoto waziache simu zao nyumbani. Hata hivyo kama wanachagua kuja na simu wanapaswa kumkabidhi Mwalimu wakati siku ya shule imeanza na hatimaye kurudishiwa siku ya shule inapofika mwisho.

Wanafunzi wanaosoma darasa la 7-9 hawatakiwi kuwa na simu zao wakati wa masomo.

## Wajibu wa kutoa ripoti

Endapo mtu anashuku kwamba mtoto anatendewa yasiyositahili yaani vibaya, wanaweza kutoa ripoti kwenye Manispaa. Inaitwa kutoa ripoti ya wasiwasi. Kwa mfano, inaweza kuwa wasiwasi kwamba mtoto anapigwa au kuwa mtoto hajapata yale matunzo yanayohitajika.

Wale wote ambao wanazo taaluma zinazohusisha kufanya kazi na watoto pamoja na vijana wanawajibika kwa kulingana na Sheria kutoa ripoti ya wasiwasi ikiwa katika utekelezaji wao kazini wanashuku kwamba mtoto anafanyiwa vibaya.

## Eneo la burudani kabla na baada ya masaa ya shule/fritidshem/fritids

Fritids inakuwa wazi siku za wiki kutoka saa kumi na mbili unusu ya asubuhi hadi saa kumi mbili unusu ya jioni: kwa masaa ya kiswidii kl. 06:30-18:30.

Watoto wana haki ya kuwa katika fritids wakati wazazi wote wawili wanafanya kazi.Unapaswa utoe taarifa mapema ni saa ngapi ambapo mtoto wako atakuwa kwenye fritids.

Mara nne katika mwaka wa masomo huwa fritids inakuwa na siku za kupanga mipango yao. Hapo ndipo kunakuwepo na watu mbadala wanaofanya kazi na shule nyingi hukuhitaji wewe mzazi utoe taarifa ya ziada ikiwa mtoto wako anahitaji kuwepo kwenye fritids hata katika siku hizi.

Endapo mtoto wako hahitaji tena nafasi ya kwendelea kuwepo kwenye fritids unapaswa utoe taarifa mapema ya kuacha, angalau siku 14 kabla ya muda uliotarajiwa.

# Kupiga picha na filamu shuleni

Wafanyakazi wanaofanya kazi shuleni wanaweza kupiga picha na kuchukua filamu zinazohusu shughuli tofauti za watoto palepale. Hii inafanywa, kwa mfano kuandika maendeleo ya mwanafunzi pamoja na kurahisisha katika kujifunza. wewe mlezi, huruhusiwi kupiga picha na kuchukua filamu shuleni.

Utapata fomu ambayo utaijaza ikiwa unaona ni sawa kwa mtoto wako picha yake kuonekana kwenye tovuti ya Manispaa na mitandao ya kijamii. Fomu hiyo inaitwa idhini/ruksa ya uchapishaji wa data ya kibinafsi, picha na filamu. Shule ya awali - darasa la 9.

# Fomu na huduma ya kielektroniki

Lishe/chakula maalum

Kufundisha lugha-zazi

Idhiniya uchapishaji/GDPR

# Taarifa za mawasiliano na shule

Härnösands
kommun